kumekucha @kumekucha @kumekucha

mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: www.kumekucha.co.tz | ISSN 4562-9710 Tol 0008 JUMANNE JANUARI 28, 2025 / Bei Tsh 1,000, Ksh. 100



# UN yampongeza Rais Dk. Samia

>> Ni katika jitihada zake za kukuza sekta ya Madini

>>Yaonesha utayari wa kusaidia VISION 2030




## TRC yaongeza safari za Treni



## DK.BITEKO AFUNGUA MKUTANO WA NISHATI

## RAIS SAMIA AIPANDISHA HADHI KIBAHA

# UN YAMPONGEZA RAIS DK.SAMIA

NA MWANDISHI WETU,

**NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa(UN)Amina Mohamed ameipongeza serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa mkakati wa kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia na utafutaji madini nchini.**

Naibu Katibu Mkuu Amina Mohamed ameyasema janao wakati wa mkutano wa pembeni wa Mkutano wa Nishati alipokutana na Waziri wa Madini Anthony Mavunde.

"Naipongeza Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia ambao umekuja na ubunifu mkubwa katika maeneo mbalimbali.Mpango wa kufanya utafiti wa kina kupitia Vision2030 ni mpango ambao tunauunga mkono kwa kuwa una lengo la kubaini madini ambayo mnayo na hivyo kujipanga vyema juu ya uvunaji wa madini hayo.

Dunia hivi sasa ina mahitaji makubwa ya madini mkakati,Tanzania imebarikiwa kuwa na madini hayo kwa uwingi hivyo suala la uongezaji thamani,utunzaji wa mazingira na kulinda jamii zinazoishi katika maeneo ya uchimbaji wa madini ni vyema yakazingatiwa wakati wa uandaaji wa mkakati maalum wa uvunaji wa madini ya kimkakati.

Umoja wa Mataifa kupitia programu zake mbalimbali za utunzaji wa mazingira ipo tayari kuunga mkono jitihada hii kubwa ya serikali ya Tanzania"amesema Mhe. Mohamed.

Akizungumza katika mkutano huo,Waziri wa Madini,Anthony Mavunde,alisema, kipaumbele cha sekta ya Madini kwa hivi sasa ni kufanya utafiti wa kina ili kuiwezesha nchi kupata taarifa za kiwango na ubora wa madini iliyonayo.

Amongeza kwamba, utafiti wa kina utaleta matokeo chanya kwenye maeneo ya kijamii na kiuchumi na hivyo kusaidia kuchochea maendeleo ya Tanzania,kwakuwa pamoja na mafanikio yote ya kwenye sekta ya madini eneo ambalo limefanyiwa utafiti ni asilimia 16% ya eneo la nchi nzima.

## RAIS SAMIA AIPANDISHA HADHI KIBAHA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ameweka wazi kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia Halmashauri ya Mji wa Kibaha kupandishwa hadhi na kuwa Manispaa.

Mchengerwa ameeleza kuwa taratibu za mwisho zinafanywa, na kutatangazwa rasmi kuwa Manispaa hivi karibuni.Ameeleza hayo katika mkutano wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani Pwani uliofanyika Mailmoja, Kibaha.

Mkutano ulioandaliwa kupongeza na kuunga mkono azimio la mkutano Mkuu maalum wa CCM uliofanyika Dodoma, kumchagua Mwenyekiti CCM Taifa Dkt Samia Suluhu Hassan kugombea kiti cha Urais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Mchengerwa alisema,tangu Rais Samia aingie madarakani, tayari ameunganisha vitongoji kuwa vijiji na vijiji kuwa miji kulingana na vigezo na utaratibu ulio wazi.

"Kwa namna mji wa Kibaha ulivyokuwa, hakuna sababu mji huu usiwe Manispaa. Rais Samia kwa kushirikiana na viongozi wa mkoa, wilaya, na jimbo, ameleta maendeleo makubwa Kibaha na Mkoani Pwani, na hayo ni manufaa ya vizazi vijavyo," alisema Mchengerwa.

Alifafanua zaidi kuwa hakuna anayekataa kwa macho kwamba Rais Samia amefanya kazi inayoonekana na ameacha alama katika sekta zote, huku wananchi wakiwa mashahidi wa maendeleo hayo.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Rufiji na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Pwani (MNEC), Mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kura, na tutaakikisha hakuna kura inayopotea wakati wa uchaguzi.

MNEC huyo aliwataka madiwani, wabunge, na wanachama wa CCM kuendelea kukisemea chama kwa kueleza utekelezaji wa ilani na miradi iliyotekelezwa.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, Silvestry Koka, alifurahi na kuishukuru Serikali kwa uamuzi huu baada ya maombi yao ya muda mrefu ya kuhakikisha mji wa Kibaha unakuwa Manispaa.

"Katika mji wetu, yaliyofanyika ni mengi kama maajabu, lakini Rais Samia anafanya maajabu zaidi. Mfano, mwaka 2010 wakati naingia madarakani, lami pekee ilikuwa kuanzia Tamco – Hospitali ya Tumbi hadi Pichandege. Leo hii, karibu kila kata ina barabara ya lami na ambazo hazijakamilika zinakwenda kutandazwa lami katika kata zote," alibainisha Koka.

Koka alieleza kuwa kwa sasa Kibaha ina hospitali ya wilaya Lulanzi, vituo vya afya, umeme kila kona, miundombinu ya barabara, na ujio wa barabara sita katika barabara kuu ya Morogoro. Pia, nishati ya umeme, maboresho katika sekta ya elimu, na maji safi vimeendelea kutekelezwa, ambapo imebakia kata ya Pangani ambayo kuna mradi unaendelea, na ukikamilika kero hiyo itakuwa historia.

"Maendeleo haya yote ni matunda ya jitihada zilizofanywa na Serikali, madiwani, jimbo, na usimamizi wa CCM, na ndio sababu ya kupanda hadhi Halmashauri yetu kuwa Manispaa," aliongeza Koka.

## DK.BITEKO AFUNGUA MKUTANO WA NISHATI

NA MWANDISHI WETU,

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,Dk.Doto Biteko, amesema Afrika inapaswa kutumia fursa zote za nishati zinazopatikana ili kupunguza upungufu wa umeme unaoathiri takriban Waafrika milioni 571.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana,katika ufunguzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati, Dk.Biteko alibainisha kuwa bara hilo linahitaji mkakati wa pamoja kufikisha huduma ya umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo 2030.

Alisema,Tanzania imepiga hatua kubwa,kutoka kuzalisha megawati 21 za umeme mwaka 1960 hadi megawati 3,160 sasa huku asilimia 61 ya nishati hiyo ikiwa safi.

Biteko alisema,mtandao wa umeme umeunganishwa na nchi jirani kama Kenya na Rwanda ambapo alisisitiza umuhimu wa uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya nishati ili kuchochea maendeleo ya viwanda, madini, na huduma za hoteli barani Afrika.

Mkutano huu pia unaakisi juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameonyesha dhamira thabiti katika kuimarisha upatikanaji wa nishati safi kwa Watanzania. Rais Samia amekuwa kinara wa kampeni za nishati safi ya kupikia, akihamasisha matumizi ya gesi asilia na teknolojia endelevu kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, ambao umechangia uharibifu wa mazingira.

Aidha mkutano huo wa Nishati Afrika ni fursa kubwa kwa Tanzania kuonyesha nafasi yake kama mshirika wa maendeleo ya bara. Kwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, Tanzania inajipanga kuwa mfano wa kuigwa katika mapinduzi ya nishati Afrika.

Kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu, Tanzania inasimama si tu kama jukwaa la maamuzi ya kimkakati, bali pia kama mshirika wa kweli wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Bara la Afrika. Njia ya kuelekea Mission 300 inafunguliwa, na Dar es Salaam inakuwa kitovu cha mageuzi haya.



# TRC yaongeza safari za Treni

NA MWANDISHI WETU

**SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limetangaza kuongeza huduma za treni za mijini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, jijini Dar es Salaam kwa siku kuanzia jana kutokana na kufungwa kwa baadhi ya barabara za kuingia katikati ya jiji kutokana na mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika.**

Kwa mujibu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano, Fredy Mwanjala imezitaja treni hizo kuwa ni ya Stesheni ya Kamata na Pugu. Mwanjala amesema treni zilizoongezwa ni ya saa 12.00 asubuhi kutoka Stesheni ya Kamata na treni ya saa 12.05 jioni kutoka Stesheni ya Pugu.

"Shirika la Reli Tanzania linapenda kuwatangazia kuwa kutokana na kufungwa kwa barabara za kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam kufuatia mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika, shirika limeongeza treni mbili za mjini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, Jijini Dar es Salaam kwa siku ya Januari 27 na 28, 2025," imeeleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, Mwanjala alisema pamoja na hatua hiyo ratiba za awali za treni zitabaki kama kawaida.




# ED MNASI AZINDUA KITABU MALEZI YA WATOTO

NA HUSNA NASSORO

**MWANDISHI wa kitabu cha Elimu na Malezi kwa Watoto Katika Zama za Kidijitali ambaye pi ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro Dkt. Haji Mnasi amezindua kitabu hicho katika kijiji cha Kitangari Sokoni kilichopo wilayani Newala mkoani Mtwara.**

Uzinduzi wa kitabu hicho umefanya juzi katika Uwanja wa Mpira Shule ya Msingi Kitangari B.Dkt.Mnasi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuamini huku akisema licha ya kuwa na majukumu mengi ya kiserikali ila aliwiwa kuandika kitabu hicho kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa utandawazi ambao umeelezwa kuathiri mila na tamaduni za taifa.

"Kitabu hicho kinaenda kuwa suluhisho katikati zama hizi za utandawazi na ukuaji wa teknolojia", alisema,Dkt. Haji Mnasi.

Hivyo Dkt. Haji Mnasi amewataka wazazi, walezi pamoja na jamii kupata nakala za kitabu hicho ili kuwasaidia watoto katika namna bora ya kujifunza na kupata elimu pamoja na malezi yaliyo bora ili kukuza taifa lenye maadili mema, uchapakazi kama ambavyo maono ya Rais Samia Suluhu yamekuwa yakijikita katika kusisitiza ujenzi wa jamii bora na kizazi salama cha kesho.

# NITASHANGAA CHADEMA IKIWARUDISHA KINA HALIMA MDEE



NA MWANDISHI WETU

**KWA Mujibu wa Katiba ya Chadema hakuna Kiongozi wa ngazi yoyote wa Chama hicho anayeweza kufanya Maamuzi ya Peke yake (Maamuzi Binafsi) ambayo yanaweza kutengua adhabu aliyopewa Mwanachama yeyote yule na Vikao halali vya Chama.**

Njia pekee ya kufanya hivyo ni kwa kutumia Vikao vile vile vya Chama, ambavyo kwa namna yoyote havitaweza kuketi ili kujadili Ujinga huo, Halima Mdee na Wenzake walishafukuzwa na Chadema kwa vikao halali vya Chama vilivyotumia pesa nyingi za Chama kuviitisha, Chadema haina hela za kuchezea ili kuitisha vikao vya masihara, hili limeisha na waendelee kujiambatanisha na CCM kama walivyofanya kwa miaka mitano yote.

Dkt Slaa aliondoka Chadema kwa kisingizio cha Lowassa, akiwa yeye ndiye kamleta Lowassa! akahongwa Ubalozi waziwazi , namna alivyoingizwa Hotelini kwa Press iliyoandaliwa na serikali ili kutukana Chadema kila mtu aliona (Video zile zingalipo hata leo).

Ni huyu Dk.Slaa hata Shambulio la kumuua Tundu Lissu aliita la kawaida, na kwamba mashambulio kama hayo hata huko Ulaya yanafanyika, huyu aweza kurudi Chadema, Chama alichokituhumu kuleta Choo sebuleni ili iweje?

Napinga kabisa jambo hili kufanyika, Chadema ina rundo la Wamama wenye uwezo mkubwa sana wa kuwa viongozi, hakuna sababu ya maana wala ya kijinga ya kuwarejesha Mamluki, Naapa kutoshirikiana nao katika lolote hata kama watarejeshwa (Maana Chama si changu peke yangu)

Wengine wanaweza kusema kwamba Nina roho mbaya na labda nashindwa Kusamehe, lakini ni wapi kwenye Vitabu vya Mungu imeandikwa Tumsamehe Shetani? Pamoja na Mwenyezi Mungu kusisitiza mno Msamaha na kusamehe lakini hakuwahi kuagiza kusamehe Mwovu Shetani.

Naomba Kuwasilisha.



# TANZANIA ITANUFAIKA VIPI MKUTANO WA NISHATI AFRIKA?

**NA MWANDISHI WETU**

MKUTANO wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika umefunguliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri Mkuu na Waziri Nishati,Doto Biteko katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Lengo la mkutano huo ni kufanikisha upatikanaji wa nishati kwa Waafrika milioni 300 ifikapo 2030, kwa kaulimbiu ya Mission 300.Kuanza kwa Mkutano huo Tanzania imeandika historia kwa kuwa mwenyeji wa tukio hilo kubwa kutokana na ugeni mkubwa wa viongozi iliowapokea kwa wakati mmoja.

Kwa kushirikisha viongozi wa Afrika, mashirika ya kimataifa, na sekta binafsi, mkutano huu si tu unaonyesha jukumu la Tanzania kama mshirika wa maendeleo ya Afrika, bali pia nafasi yake ya kipekee katika mapinduzi ya nishati.

**Tanzania Itanufaika Vipi?**

1. Uwekezaji wa Miundombinu ya Nishati

Mkutano huu unatarajiwa kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika miradi ya nishati jadidifu, hususan umeme wa jua, upepo, na gesi asilia. Tanzania, ikiwa na vyanzo vingi vya nishati, itakuwa na nafasi ya kuonyesha uwezo wake wa kuzalisha na kusambaza nishati safi kwa bei nafuu, si tu kwa matumizi ya ndani, bali pia kwa kuuza nje.

**2. Uhamasishaji wa** Ajira na Uchumi

Miradi ya nishati inayotarajiwa baada ya mkutano huu itafungua fursa za ajira kwa Watanzania, hususan vijana, katika sekta za ujenzi, teknolojia, na huduma. Hii itachangia katika kuongeza pato la taifa na kuboresha maisha ya wananchi.

**3. Mazingira Bora ya Kibiashara**

Kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu, Tanzania inajiweka kama kitovu cha mijadala ya maendeleo ya nishati Afrika. Hili litachangia kuimarisha taswira ya taifa kwenye jukwaa la kimataifa na kuvutia washirika wa maendeleo.

**4. Kupambana na** Umasikini wa Nishati

Zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wanategemea kuni na mkaa kwa kupikia. Mkutano huu utakuwa na jukumu la kuimarisha mipango ya serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi na endelevu kwa wananchi wote.

Rais Samia Suluhu Hassan: Kinara wa Nishati Safi

Mkutano huu pia unaakisi juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameonyesha dhamira thabiti katika kuimarisha upatikanaji wa nishati safi kwa Watanzania. Rais Samia amekuwa kinara wa kampeni za nishati safi ya kupikia, akihamasisha matumizi ya gesi asilia na teknolojia endelevu kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, ambao umechangia uharibifu wa mazingira.



Chini ya uongozi wake, Tanzania imepiga hatua katika miradi ya nishati safi, ikiwa ni pamoja na kupanua usambazaji wa gesi majumbani na kuzindua mipango inayolenga kupunguza uchafuzi wa mazingira. Jitihada hizi zimeifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika na kumpa Rais Samia heshima kubwa kama kiongozi mwenye maono ya maendeleo endelevu.

Hitimisho

Mkutano wa Nishati Afrika 2025 ni fursa kubwa kwa Tanzania kuonyesha nafasi yake kama mshirika wa maendeleo ya bara. Kwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, Tanzania inajipanga kuwa mfano wa kuigwa katika mapinduzi ya nishati Afrika.

Kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu, Tanzania inasimama si tu kama jukwaa la maamuzi ya kimkakati, bali pia kama mshirika wa kweli wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Bara la Afrika. Njia ya kuelekea Mission 300 inafunguliwa, na Dar es Salaam inakuwa kitovu cha mageuzi haya.

# Trump anaifundisha Afrika kujikomboa

NA MWANDISHI WETU

**UTU wetu na thamani yetu, ilishuka miaka mingi, baada ya kuukumbatia ulemavu wa kusaidiwa.Tukubaliane waafrica, kuna ujinga fulani tumeushikilia, tungekuwa watu wa kuendelea kupitia misaada, tungeshatoka hapa tulipo.**

Ukweli ni kwamba, misaada mingi ya magharibi haijawasaidia walengwa wa misaada hiyo zaidi ya kuishia mifukoni mwa watu wachache.Nitamshangaa Prof. Anna Tibaijuka, kuulizia Ukimwi ulianzia wapi?.Ukimwi ulianzia Marekani,Kama ulianzia huko, ni kwa nini Umeua na kuteketeza waafrica wengi zaidi??.

Motive ya kutengeneza,hivi virusi ilikuwa ni nini?.

Ukiisoma, na kuielewa Sayansi ya Kirusi kinavyoingia,kuathiri Chembe hai ya kinga ambayo ni ( Commander in chief), inayotoa amri, kwa chembei kinga nyingine, Lazima ukubaliane nami kuwa, maarifa ya binadamu ya " Genetic engineering yalifanya kazi.Dunia ina mengi ya kushangaza, Ngoja tujadiri tutawasaidiaje ndugu zetu wanaohitaji dawa hizi.

1) Kwa waafrica wote hii ni agenda yetu sote.a) Tu mobilise Resources,zetu tuwe na ushirika na wenye kupenda ushirika nasi, tujenge viwanda vyetu vya madawa, hata ikibidi kuwapeleka wana wa kiume na wa kike wa kitanzania, Kenya na nchi nyingine kupata maarifa ya juu zaidi ya kinga mwili( immunology).

b) Kila nchi inaweza kubeba jukumu moja moja, wakati Kenya wana tengeneza chanjo, sisi tujenge viwanda vya ARV.

2) Tuweke nguvu kwenye kukinga zaidi.a) Panaweza kuwa na vipimo vya kucheck kabla watu hawajaingiliana.b) Tutengeneze viwanda vya kuzalisha Condom nyingi.

C) Mtu anposhtuka kayatimba, basi guest zote ziwe na dawa za kuzuia kirusi hicho kusambaa( Post exposure prophylaxis).

d) Ngono duniani kote baadhi ya maeneo imekuwa ni commodity, basi kuwe na Priority kwenye nchi za kusaidia makundi yaliyoathirika kiuchumi, wapewe mikopo nafuu( serving disadvantaged societies),Ili ku shift equilibrium ya biashara ya ngono, kuja kwenye biashara nyingine.

3) 1,2, hapo juu zinaweza ku apply kama long term plan, short term plan ni kama hizi.a) Tupunguze matumizi.

Badala ya magari ya mil 600, tununue magari ya mil 60!, b) Tuwe na mfuko wa Taifa wa Ukimwi i) 10% ya mauzo ya kodi yaende kwenye mfuko huu.

ii)Tuhamasishe matumize ya Teleconference, badala ya kulazimisha watu kusafiri kwa kuchoma mafuta ya petrol kwa ma V8 ili tuwe na hela ya emergency kwa ajili ya mfuko huu, badala ya kuitumia kununulia mafuta ya magari.

iii) 7% ya mapato ya mashindano yote kwenye mpira iende kwenye mfuko wa Taifa wa Ukimwi.Ninajaribu kuonyesha tu kuwa, hili tatizo liko ndani ya uwezo wetu!, Trump kutunyima misaada, ni NIA njema, ya kutaka tushtuke, tutumie raslimali zetu kwa faida ya watu wetu na si vikundi vya watu.

**TUKATAE ULEMAVU WA KUSAIDIWA.**
**Isaya.**





# NINGEKUWA CHALAMILA NINGEJIUZULU KULIKO KUSUBIRI KUTUMBULIWA



**NIMESIKILIZA utetezi wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,Albert Chalamila,kuhusu kauli yake kwamba yule mama mjamzito aliyemwambia kama hatoi Tshs 50,000 achukue bajaji aende kwa mume wake atumie kisu na mikasi kumzalisha ni wa hovyo.**

Ni utetezi usio na lojiki na ambao hata mtu asieenda shule angeweza kufanya vizuri zaidi.

Ni afadhali hata angekaa kimya. Chalamila amejiumauma tu wala hakuna alichosema cha maana kutuambia kwa nini, yeye kama kiongozi mwakilishi wa Raisi, alitoa kauli kama ile ya kubeza.

Kudhalilisha na hata kumtukana mama ambaye alikuwa akimlilia kuhusu kulazimishwa kutoa Tshs 50,000 ili apewe huduma ya kujifungua ni ukatili wa kijinsia.Ni ngumu kuamini utetezi ule umetolewa na msomi mwenye Masters.

Chalamila anagusia kwamba huyu mama mjamzito alishindwa kulipa Sh.50,000 kwa sababu alimaliza fedha kwenye ngoma za vigodoro! In fact, hayo ni matusi kwa watu wasio na uwezo kwamba wanashupalia ngoma ndio maana hawawezi kumudu gharama za matibabu!

Ushauri wangu kwa Chalamila ni kwamba aache kiburi. Aombe msamaha kwa huyo mama mjamzito, kwa mume wake,kwa Rais Samia Suluhu Hassan na kwa Watanzania wote kwa ujumla.Kwa kauli yake ili nilitarajia angeandika barua ya kujiuzulu kwa Raisi Samia badala ya kusubiri kuondolewa.

Kuendelea kujitetea ni kuwaambia wananchi alichosema ndio msimamo wa serikali ya Samia.Kama huna hela ya kuchangia kujifungua mwambie mumeo achukue kisu na mikasi akuzalishe!Natamani kuona PDF ya Rais Samia ikifanya mabadiliko ya kumtumbua au kumuhamisha ikisambaa.

MAKALA JUMANNE, JANUARI 28-29, 2025

# MIAKA 65 MAISHA YA RAIS SAMIA NA SAFARI YAKE YA KUSISIMUA

Na Bwanku M Bwanku.

**JANUARI 27 mwaka huu Taifa letu lilisherehekea miaka 65 toka kuzaliwa kwa Rais wa sasa wa Awamu ya 6 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dkt. Samia Suluhu Hassan, anayehudumu kwa mara ya kwanza kwenye nyadhifa ya juu kabisa nchini toka achukue mikoba hiyo Machi 19, 2021 baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya 5 Hayati John Pombe Magufuli.**

Kwa wasiyemfahamu sana, Rais Samia, ndiye Mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kushika nafasi ya Urais wa Tanzania baada ya pia kuwa Mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Makamu wa Rais mwaka 2015 hadi 2021, nafasi kuu za juu kabisa katika Taifa letu.

Rais Samia Suluhu Hassan alizaliwa Januari 27, 1960 katika Kijiji cha Kizimkazi kilichopo Jimbo la Makunduchi, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja Visiwani Zanzibar, kabla ya kuanza masomo yake ya Msingi katika shule mbalimbali ikiwemo Shule ya Msingi Chwaka kuanzia mwaka 1966 hadi 1968, kisha Ziwani mwaka 1970 na baadae Shule ya Msingi Mahonda mwaka 1972.

Baadae akajiunga Sekondari ya Ng'ambo kwa masomo ya kidato cha kwanza hadi cha tatu kisha Shule ya Sekondari Lumumba alikomaliza Kidato cha nne mwaka 1976.

Kwa maelezo yake mwenyewe Rais Samia wakati akihojiwa na Kituo cha Habari cha TBC, kuanzia Shule ya Awali mpaka anafika Kidato cha nne alisoma kwenye shule zaidi ya 10 na anataja sababu ya hiyo kutokea ni kwasababu Baba yake Mzazi alikuwa Mwalimu kwahiyo alipokuwa anahamishwa kwenye vituo vya kazi na yeye alihama na familia yake kwenda kwenye Shule au eneo alilohamishiwa Baba yake.

Kwa mara ya kwanza Rais Samia anasimulia aliajiriwa mwaka 1977 katika Ofisi moja ya kwenye Wizara ya Mipango na Maendeleo- Zanzibar akiwa na umri mdogo sana wa miaka 17 lakini alirudishwa nyumbani baada ya kuonekana kuwa na umri mdogo lakini baadae aliitwa tena kufanya kazi eneo hilo na ndiyo ilikuwa ajira yake ya kwanza na mwanzo wa safari yake ya Utumishi wake katika Ofisi hiyo ya Maendeleo.

Baadae alijiendeleza kimasomo kwa kusoma Ngazi ya Cheti (Certificate) alipohitimu mwaka 1983 kwenye masuala ya Uchumi na Takwimu kwenye Chuo cha Uchumi Zanzibar na ndipo alipoajiriwa kufanya kazi kwenye Wizara ya Mipango na Maendeleo mwaka 1983 hadi 1986 na baadae kwenda Chuo Cha Maendeleo ya Uongozi Mzumbe (IDM) kufanya Advanced Certificate ya Utawala, kabla ya kwenda kusoma Kozi ndogondogo za miezi mitatu mitatu kwenye Chuo cha Utawala wa Umma kule Lahore, Pakistan mwaka 1987, kisha Taasisi ya Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI) mwaka 1991 na Taasisi ya Uongozi ya Hyderabad, India mwaka 1998 kwa ajili ya Astashahada ya Utawala.

Baadaye, alikwenda sasa Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza alikosoma Undergraduate Diploma ya Uchumi kisha akafanya Masters Degree (Uzamili) kwenye Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Southern New Hampshire, Marekani.

Kama nilivyoanza kueleza pale juu kidogo, mwaka 1977 aliajiriwa akiwa Karani Masijala lakini kwa maelezo yake mwenyewe, aliona pale sio mahali pake maana alikuwa anafanya kazi zaidi ya aliowakuta pale.

Alifanya kazi hata zile zilizofanywa na watu wa Juu wenye vitengo na ndio maana akaamua kwenda kuongeza elimu ili aendelee zaidi na baada ya kuongeza elimu kama nilivyoeleza pale Juu ndipo akaajiriwa na Shirika la Chakula Duniani (World Food Program) kwenye project zao mbalimbali pale Zanzibar, akafanya hapo kazi kwa miaka 9 kuanzia mwaka 1988 hadi 1997.

Baada ya kutoka Umoja wa Mataifa kwenye Shirika la Chakula Duniani, akaingia sasa kwenye Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO's) akafanya kazi kubwa sana kuziendeleza ukuzaji wake wa NGOs za Zanzibar mpaka kuwa Mkurugenzi wa kwanza wa Taasisi zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA) mwaka 1995 mpaka mwaka 2000 huku akifanya shughuli zingine mbalimbali.

Akashika nafasi zingine kama Mlezi wa Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Zanzibar kutoka mwaka 1997 hadi 2000, Mjumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fursa sawa kwa wote-EOTF kutoka 1996 hadi 2000, Mwanachama wa Lions Club Zanzibar kutoka 1991 hadi 1998.

Mjumbe wa Kamati ya Uundaji wa Sera ya Elimu Zanzibar mwaka 1996, Mwanachama Mwanzilishi wa Taasisi ya Kuchochea Maendeleo ya Wanawake Zanzibar kutoka 1991 hadi 1994 na nafasi zingine kama Mjumbe wa Kamati ya Msamaha wa Wafungwa (Parole Committe).

Baada ya safari yote ya elimu ndani na nje ya nchi, kuzunguka kote huko na kufanya kazi kubwa na nzito kwenye Serikali, Taasisi za Kimataifa, NGO's na Taasisi zingine.

Hatimaye mwaka 2000 ndipo akapata mawazo ya kuingia kwenye Siasa na sababu moja tu anasema iliyomvuta kuingia kwenye Siasa, ni kwamba alikuwa anaangalia Baraza la Wawakilishi ile mijadala inavyoendelea, kama inavyofahamika Zanzibar upinzani umepamba moto kwahiyo kilichomsukuma ni kuingia tu kule nikasaidie kupeleka hoja za Wananchi na kuisimamia Serikali.

Mwaka 2000 akajitosa kwenye Siasa na kufanikiwa kushinda kuwa Mbunge wa Viti Maalum vya Wanawake baada ya watu wengi kwenye Mkoa wake wa Kusini Unguja kumkubali sana baada ya kazi kubwa aliyoifanya ya kuwasaidia Wananchi wakati akiwa na Shirika la Chakula Duniani kusaidia masuala ya chakula kwa wingi kwenye eneo hilo baada ya kuwa na uhaba wa chakula.

Akaingia Baraza la Wawakilishi na Rais wa Zanzibar wa wakati huo Abeid Amani Karume akamteua kuwa Waziri katika Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ambako alifanya kazi kwa miaka mitano mpaka 2005.

Wananchi waliendelea kumuamini kuwa Mbunge wa Viti Maalum na kisha tena 2005, Rais Karume akaendelea kumuamini na kumteua kuwa Waziri kwenye Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ambako nako alihudumu kwa miaka mitano bila kubadilishwa wala kutumbuliwa mpaka 2010.

2010 kwenye Uchaguzi Mkuu akaamua kuachana na Ubunge wa Viti Maalum na kwenda kugombea Ubunge wa Jimbo kwenye Jimbo la nyumbani Makunduchi na kushinda kama kawaida yake na sasa kuwa Mbunge wa Jimbo na si tena wa Viti Maalum na kuingia moja kwa moja kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa akateuliwa kuwa Waziri kwenye Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano mpaka mwaka 2015. Mwaka 2014 wakati Taifa likipambana kupata Katiba Mpya na Rais wa kipindi hicho wa Awamu ya 4 Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kuunda Bunge Maalum la Katiba.

Bunge la nyumbani la Wawakilishi la Zanzibar likampendekeza kuwa Msaidizi wa Bunge la Katiba na hivyo yeye kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba na Hayati Samwel Sitta ambaye alikuwa Spika wa Bunge la Tanzania akiwa Mwenyekiti wa Bunge lile la Katiba.

Ilipofika mwaka 2015 wakati Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikimsimamisha Hayati John Pombe Magufuli kuwa Mgombea Urais wa Tanzania kupitia CCM, Kamati Kuu ya CCM chini ya Mgombea mwenyewe wa CCM Hayati Dkt. John Pombe Magufuli walimteua yeye kuwa Mgombea Mwenza wa Mgombea Urais wa CCM na baada ya CCM kushinda kwenye Uchaguzi Mkuu ule wa mwaka 2015 ulimfanya yeye moja kwa moja kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania chini ya Hayati Magufuli.

Akiwa Mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo ya juu ya pili kwenye uongozi wa nchi yetu kabla ya Machi 17, 2021 ambapo aliyekuwa Rais, Hayati Magufuli alipofariki dunia na yeye kuwa rasmi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mpaka sasa, Tanzania ikisherehekea miaka 65 ya maisha yake toka kuzaliwa mwaka 1960, maisha ya Rais Samia Suluhu Hassan yamekuwa ya Utumishi tosha kwa watu huku akifanya kazi nyingi sana ndani ya nchi kwenye Taasisi zisizo za Kiserikali, ndani ya Serikali kwenye nyadhifa kubwa kubwa na nzito Kitaifa pamoja na kazi kubwa alizozifanya Nje ya Nchi hasa kwenye Shirika la Chakula Duniani.



Maisha yake yamekuwa msisimko tosha, darasa na inspirational tosha kwa watoto wa kike na Wanawake kuamini kwamba Wanawake ni Jeshi kubwa na kwa vijana kuamini kwamba kila kitu kinawezekana chini ya jua iwe umetoka kwenye familia maskini, uwe wa Jinsia yoyote ile na mengine.

Jambo la muhimu ni kuweka malengo yako na kufanya kazi kwa bidii na kujituma. Historia yake imejaa upekee na uimara wa Wanawake kwani licha ya yote lakini Rais Samia ameweza kuhimili mpaka sasa akiwa Mkuu wa Nchi iliyotoka kwenye majanga ya kuondokewa na Mkuu wake wa nchi na majanga ya maradhi ya Uviko-19 lakini bado Taifa liko imara.

Kwenye Chama chake cha siasa (CCM) ambacho ni moja ya Chama kikubwa kabisa cha Siasa Barani Afrika na Duniani kwa ujumla, Rais Samia ameshika nafasi nyeti sana na za juu kabisa kabla ya sasa yeye mwenyewe akiwa ndiye Mkuu wa Chama kama Mwenyekiti wa Chama hicho. Amepita kwenye nafasi mbalimbali nyingi na kubwa sana ndani ya Chama toka ajiunge nacho mwaka Juni 10, 1987.

Ndani ya CCM, Rais Samia kabla ya sasa kuwa Mkuu wa Chama hicho kama Mwenyekiti, amewahi pia kushika nafasi za juu kabisa ndani ya Chama ambazo zingine anaendelea kuzishika mpaka leo kama kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, nyadhifa alizonazo mpaka sasa. Nyadhifa hizi ni za juu sana na zote zikiwa ndizo zenye maamuzi ndani ya CCM.

Pia amewahi kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Mjumbe wa Kamati za Siasa Mkoa na Wilaya ya Kusini Unguja, Mwanachama wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) na zaidi kushiriki kwenye tukio muhimu na nyeti la kuandika Ilani ya CCM mara 4 mfululizo kuanzia mwaka 2005/2010, 2010/2015, 2015/2020, 2020/2025.

Toka ashike usukani wa kuliongoza Taifa amefanya mageuzi makubwa sana ya maendeleo ikiwemo uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo, kushusha fedha za miradi kila mahali na mengine mengi.

Akiwa na miaka mitatu pekee katika uongozi, tayali Rais Samia ametunukiwa Shahada 4 za Heshima (Honoris Causa) na Vyuo Vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Walianza UDSM Novemba 30, 2022 kumtunuku Shahada ya Juu ya Heshima kwenye Humanitia na Sayansi Jamii (Social sciences), Oktoba 10, 2023 wakafuata Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha nchini India.

Desemba 28, 2023 Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) kumtunuku Shahada nyingine ya Uzamivu ya Usimamizi wa Utalii na Masoko (Doctor of Philosophy in Tourism Management and Marketing- Honors Causa) na kisha Chuo Kikuu kikubwa cha Ankara cha nchini Uturuki kumtunuku tena Rais Samia Udaktari wa Heshima.

Si jambo linalotokea mara nyingi kwa kiongozi mmoja ndani ya Taifa kutunukiwa Shahada 4 za Heshima kwa mpigo ndani ya muda mfupi wa uongozi wake. Wote tunakumbuka Hayati Rais Magufuli wakati wa uongozi wake wa Awamu ya 5 alitunukiwa mara moja Shahada ya Heshima na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) mwaka 2019 na Mstaafu Rais wa Awamu ya 4 Jakaya Kikwete pia mwaka 2011 alitunukiwa mara moja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Kwa miaka ya karibuni, anakuwa Rais wa kwanza wa kizazi kipya wa Tanzania kutunukiwa Shahada ya Heshima na Chuo kikubwa chenye heshima kubwa duniani cha Jawaharlal Nehru cha India huku akiandika historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kutunukiwa Shahada ya Heshima na Chuo hicho na Rais wa 3 pekee baada ya Rais wa Urusi, Vladimir Putin pamoja ya Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Japan Hayati Shinzo Abe kutunukiwa na Chuo hicho.

Ndani ya miaka mitatu, Rais Samia ameshatunukiwa Shahada 4 za Udaktari wa Heshima pamoja na Tuzo na kutajwa kwa zaidi ya mara 5 kutoka kwa majarida na taasisi mbalimbali kubwa za kimataifa kwa kutambua kazi yake kubwa anayoifanya kusukuma maendeleo kwenye Taifa lake.

Tayali Jarida maarufu la Avance Media la Ghana lilimtaja kama mmoja wa Wanawake 100 wa Afrika wenye nguvu na ushawishi mkubwa Barani Afrika kabla ya Majarida mengine makubwa yanayosomwa duniani kote kama The Time na Forbes ya Marekani kumtaja pia miongoni mwa Wanawake 100 wenye nguvu ulimwenguni.

Chama Cha Waandishi wa Habari za Miundombinu na Fedha Afrika (MIFA)wakamchagua na kumpa Tuzo pia Rais Samia kama Rais aliyefanya mapinduzi makubwa zaidi ya miundombinu Barani Afrika kwa mwaka 2022.

Haya yote yanafanywa kwa kutambua jitihada zake kubwa za kuendeleza mageuzi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kupitia mtindo wake wa uongozi unaoamini katika 4R kama maridhiano katika kujenga Taifa imara na la pamoja.

Uamuzi huu ni wa kutambua uongozi wa kipekee wa Rais Samia katika kuendeleza mageuzi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi nchini Tanzania.

Mageuzi hayo yameboresha ustawi wa Watanzania, kukuza sifa ya Tanzania duniani kote na kuendeleza uhusiano wa kibiashara,kiuchumi na kisiasa kati ya Tanzania na nchi nyingine kote duniani na ndiyo maana kuanzia Januari 27-28, 2025 Tanzania kunafanyika Mkutano wa Nishati wa Dunia na Viongozi wakuu wa nchi zaidi ya 30 wako nchini na ulimwengu mzima kujadili masuala ya nishati.

Hii yote ni ushawishi mkubwa wa Rais Samia kwasasa kwenye siasa za ulimwengu.

Nje ya maisha yake toka kuzaliwa, elimu na utumishi, Rais Samia ameolewa na Bwana Hafidh Ameir na wamejaaliwa watoto wanne, watatu wakiwa wakiume na mmoja wa kike.=Huyu ndiye Mwanamke wa Shoka, asiyelaza zege, Muumini wa Vitendo kuliko maneno, mbeba maono na Msikivu kwelikweli ambaye tunasherekea miaka yake 65 iliyotukuka.

**MAKALA HII IMEANDIKWA NA BWANKU M BWANKU AMBAYE NI AFISA TARAFA YA KATERERO ILIYOPO BUKOBA MKOANI KAGERA.***

# HIVI NDIVYO WERUWERU INAVYOELEKEA KUWA JANGWA

NA MWANDISHI WETU

**PICHA ya Kata ya Weruweru inavutia machoni mwa kila anayeitembelea kwa mara ya kwanza.Kijani kibichi kinachozunguka vijiji vinne vya kata hiyo (Kikavu Chini, Longoi, Ngosero, na Mbatakero kwenye mashamba na milima, kinasababisha mgeni kuhisi kuwa ameingia katika Bustani ya Eden.**



Hata hivyo, hali hiyo ya amani na uzuri inatoweka haraka unapozunguka vijiji vya kata hii na kufika kwenye kingo za mito inayozunguka maeneo hayo. Huko, ukataji miti hovyo unafichua sura nyingine ya uhalisia.

Maafa yanayojitokeza kila mwaka kutokana na mafuriko yanayoathiri wakazi, mashamba na miundombinu.Kata ya Weruweru, iliyozungukwa na mito inayochukua maji kutoka kwa Mlima Kilimanjaro, ni moja ya maeneo yaliyo na ardhi yenye rutuba na uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao.

Hii inawafanya wakazi wake kuwa miongoni mwa wakulima bora zaidi nchini.Hata hivyo, uzuri huu wa asili unakabiliwa na tishio kubwa la mafuriko yanayozidi kuongezeka kila mwaka.

Mafuriko: Historia ya Maafa Yanayorudiarudia

Mafuriko katika Kata ya Weruweru hayajawa tu matukio ya bahati mbaya. Yalianza kidogo mwaka 1960, lakini kadiri miaka ilivyoenda, madhara yake yalizidi kuwa makubwa. Mnamo mwaka 1995, mafuriko yaliharibu mashamba, makazi, na miundombinu kwa kiwango kikubwa. Hali ilirudiwa tena mwaka 1998, na wananchi walijikuta wanapoteza mali zao. Hata hivyo, mafuriko ya mwaka 2021 yamekuwa miongoni mwa makubwa zaidi.

Abradha Juma, mkazi wa kijiji cha Kikavu Chini, anasema kuwa mafuriko ya Aprili 22, 2021, yalikuwa na madhara makubwa kuliko mengine yote aliyoshuhudia katika maisha yake. Mito ilijaa, mashamba yalizamishwa, mifugo ilikufa, na nyumba za wananchi zilijikita chini ya mafuriko, huku wakazi wakiwa hawana pa kwenda.

Ukataji Miti: Sababu kuu ya Mafuriko na Uharibifu wa Mazingira

Jambo linalosikitisha ni kwamba, wakati wanajitahidi kulima na kupata chakula cha familia zao, wakazi wa Weruweru pia wanashiriki katika ukataji miti ovyo, jambo ambalo linachangia kwa kiwango kikubwa uharibifu wa mazingira.

Ikiwa miti ni nguzo muhimu ya kudhibiti mmomonyoko wa ardhi, uharibifu wake umeondoa kinga ya asili ya maeneo hayo, hivyo kuruhusu mafuriko kuharibu kila kitu kilichojengwa kwa bidii.

Ukosefu wa elimu kuhusu umuhimu wa miti na udumishaji wa mazingira umejenga mazingira ya hatari kwa jamii ya Weruweru.Wajibu wa Serikali na Taasisi za Usimamizi wa MazingiraKatika changamoto hii, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linakosolewa kwa kutotekeleza vyema Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

Sheria hii inazuia shughuli yoyote ya kibinadamu kufanyika katika maeneo ya vyanzo vya maji, lakini utekelezaji wake umebaki kuwa kiduchu. Benjamin Dotto, Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini, anasisitiza kuwa taasisi yao imejitahidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kukata miti, na kwamba wamekuwa wakifanya juhudi za kudhibiti shughuli zisizozingatia sheria karibu na mito.

Ingawa vyombo vya habari na viongozi wa vijiji wamekuwa wakitoa elimu, bado kuna pengo kubwa katika utekelezaji wa sheria.Lakini si NEMC pekee inayoshutumiwa. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) pia unalaumiwa kwa kushindwa kuchukua hatua madhubuti dhidi ya wahalifu wa mazingira.

Hali ya rushwa na upendeleo, ambapo baadhi ya watumishi wa TFS wamekuwa wakionyesha kutojali sheria kwa kuachia watuhumiwa wa uharibifu wa mazingira kutokana na maslahi yao binafsi, inazidi kuwa kikwazo.

Hata maafisa wa TFS walipoulizwa kuhusu ukataji miti katika maeneo ya Weruweru walikiri kwamba hawafahamu chochote, kwa sababu hiyo miti haiku kwenye orodha ya misitu ya taifa na suala hilo liko chini ya viongozi wa serikali za mitaa.

Hali ya Hatari: Mafuriko na Uharibifu wa Mazingira unaendelea Kuongezeka

Hali inaonekana kuwa mbaya zaidi kwani tafiti zinadhihirisha kwamba uharibifu wa mazingira utaendelea kutishia maisha ya wakazi wa Weruweru ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Wataalamu kutoka Bonde la Mto Pangani (PBWB) wanasema kuwa wanajitahidi kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira, lakini bado kuna uhitaji mkubwa wa ushirikiano wa wananchi katika kutekeleza sheria na kanuni zinazohusiana na mazingira.

Hadi sasa, wanajitahidi kufanya misako ili kuwakamata waharibifu wa mazingira, na wamefanikiwa kuwafikisha watu watano (5) mahakamani kwa uharibifu wa mazingira.

Wito wa Kuokoa Weruweru: Maisha ya Wananchi Yanategemea Hatua za Haraka

Ni dhahiri kuwa usimamizi bora wa mazingira, kuzingatia sheria na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari za mafuriko na uharibifu wa mazingira ni muhimu ili kuokoa Kata ya Weruweru na maeneo mengine yanayokumbwa na mafuriko.

Hii ni vita dhidi ya asili na watu wanapaswa kuchukua jukumu lao la kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Taasisi mbalimbali, kutoka NEMC hadi TFS na PBWB, zinajitahidi, lakini bado kuna pengo kubwa.

Wananchi wa Weruweru wanahitaji msaada wa haraka kutoka kwa viongozi wao, ili mazingira ya kata hiyo yarejee katika hali ya ustawi kama ilivyokuwa zamani.

Nini hatma ya Weruweru? Je, itabaki kuwa Bustani ya Eden, au itakuwa historia ya jangwa na maafa? Majibu yanategemea hatua za kila mmoja wetu katika kulinda mazingira.



# Kepteni Ibrahim Traoré ndiye gumzo Afrika

NA MWANDISHI WETU

**THOMAS Sankara, mwanamapinduzi na rais wa Burkina Faso kati ya mwaka 1983 na 1987, alikuwa zaidi ya kiongozi wa kawaida.Alikuwa sauti ya matumaini kwa Waafrika waliokuwa wakihangaika na mizigo ya ukoloni mamboleo na ubeberu wa mataifa ya Magharibi.**

Sankara, ambaye mara nyingi huitwa "Che Guevara wa Afrika," aliongoza nchi yake kwa miaka minne tu, lakini athari zake zimeendelea kuishi kwa vizazi hadi leo.Katika kipindi kifupi cha uongozi wake, Sankara aliwapa watu wa Burkina Faso maono ya nchi huru, inayojitegemea, na yenye ustawi.

Sankara aliamini kuwa elimu ni ufunguo wa maendeleo. Katika kipindi chake, aliweka juhudi kubwa kuhakikisha kuwa watoto wa Burkina Faso wanapata elimu bora.Alifanikiwa kuongeza kiwango cha wanafunzi mashuleni kwa asilimia 6, juhudi ambazo zilikuwa ngumu kwa nchi masikini yenye rasilimali chache.


Hili ni moja ya mafanikio makubwa ya uongozi wake.Sankara alizindua kampeni kubwa ya chanjo, na kufanikisha kuwapatia watoto milioni 2.6 chanjo za kupambana na magonjwa kama pepopunda, surua, na homa ya ini. Kampeni hiyo iliwasaidia maelfu ya watoto kuepuka vifo vya mapema.

Kutokana na hali ya kijiografia ya Burkina Faso, ambayo iko katika ukanda wa Sahel na mara nyingi hukumbwa na ukame, Sankara alizindua kampeni ya upandaji miti.Alifanikiwa kupanda miti milioni 10, juhudi zilizolenga kupambana na jangwa na kuhifadhi mazingira.

Sankara aliongoza harakati za kuikomboa Burkina Faso kutoka kwenye utegemezi wa Kifaransa.Alikataa misaada ya kifedha kutoka kwa nchi za Magharibi, akisisitiza kuwa misaada hiyo ilikuwa njia ya kudumisha utegemezi.

Alihamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii na kujitegemea.Katika jamii iliyokuwa imegubikwa na mila za kuwalazimisha mabinti kuolewa wakiwa wadogo, Sankara alianzisha kampeni kali ya kupinga ndoa za kulazimishwa.

Alitetea haki za wanawake, akiwataka kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi.Sankara alijenga reli, barabara, na shule nyingi nchini humo yote haya yalifanyika bila msaada wa nchi za nje.



Miradi yake ya maendeleo iliwafanya watu wa Burkina Faso kushikamana na kuamini kuwa nchi yao inaweza kufanikisha maendeleo bila msaada wa Magharibi.

Sankara alitofautiana sana na viongozi wengine wa Afrika ambao mara nyingi walijipendelea na kujilimbikizia mali. Aliweka mfano wa uongozi wa unyenyekevu.

Alikataa picha yake kuwekwa kwenye ofisi za serikali. Alipunguza mishahara ya viongozi wa serikali, ikiwemo wake mwenyewe. Aliendesha gari ya kawaida badala ya magari ya kifahari. Alikataa kabisa matumizi ya ndege za kifahari kwa safari za nje.

Kwa mafanikio yake yote, Sankara alikabiliana na changamoto kubwa uhasama kutoka kwa mataifa ya Magharibi na wasaliti wa ndani.Mnamo Oktoba 15, 1987, Thomas Sankara aliuawa katika mapinduzi ya kijeshi yaliyopangwa na rafiki yake wa karibu, Blaise Compaoré.

Compaoré, aliyesaidiwa na Wafaransa, alichukua madaraka na kuiongoza Burkina Faso kwa miaka 27.Uongozi wake ulijaa madai ya ufisadi na ukandamizaji, tofauti kabisa na maono ya Sankara ya nchi huru, yenye haki, na yenye ustawi.

Miaka mingi baada ya kifo chake, Thomas Sankara bado anakumbukwa kama shujaa wa Afrika.Alikuwa kiongozi mwenye maono makubwa, aliyepigania heshima ya bara lake dhidi ya ubeberu wa Magharibi. Kupitia juhudi zake, alionyesha kuwa maendeleo yanawezekana hata kwa mataifa masikini ikiwa tu kuna uongozi wa kujituma, uwazi, na uzalendo.



# Njia tano za kuondokana na uchovu na kuboresha usingizi

**Siri ya kuhisi vizuri baada ya usingizi mzuri wa usiku inaweza kuwa katika kuamka.Hapa kuna mbinu tano na vidokezo juu ya jinsi ya kuboresha usingizi wako nakupunguza uchovu.Je unahisi uchovu? Hauko peke yako - na pengine hiyo ndio sababu uunashangaa ni jinsi ya kubadilisha tabia yako ya kulala.**

Mara nyingi, mikakati tunayokumbushwa ambayo inaweza kutusaidia kujisikia raha zaidi imezingatia mikakati ya usiku, kama vile kuweka wakati wa kulala na kutokuwa na shughuli nyingi kwenye simu yako.

Lakini kupata usingizi mzuri wa usiku sio tu kuhusu tabia za usiku. Na kuhisi furaha sio kila wakati kunahusiana na usingizi mzuri wa usiku. Kuna mambo mengine unayoweza kufanya mapema katika siku, wakati unapohisi una uchovu wa macho au ambayo yanaweza kuwa na athari.

Kufuatilia viwango vyako vya madini ya chuma mwilini

Mtu mmoja kati ya watatu duniani kote hana viwango vya kutosha vya madini ya chuma mwilini. Hasa makundi ya watu walio katika mazingira magumu wako hatarini, kama vile watoto wadogo na wazee, wasichana na wanawake wa umri wa kuzaa - ambao hupoteza damu wakati wa hedhi - wanawake wajawazito, wanariadha ambao hufanya michezo ya nguvu, watu wasiokula nyama na watu wanaochangia damu mara kwa mara.Lakini mtu yeyote anaweza kuteseka na upungufu wa chuma au matokeo yake, hali inayojulikana kama anemia. Dalili ni pamoja na uchovu , lakini pia inaweza kujumuisha hali ya kutokuwa na utulivu na kuamka amka usiku.

Ikiwa unahisi uchovu kila wakati, licha ya kubadilisha tabia yako ya kulala, unaweza kuhitaji ushauri wa daktari wako kuhusu viwango vyako vya ferritin (aina ya protini ambayo husaidia kuhifadhi chuma) au hemoglobin, ambayo hubeba oksijeni karibu na mwili.

Hata kama huna upungufu wa chuma, unaweza kuiepuka kwa kuzingatia lishe yako. Vyanzo vya chuma vilivyoingizwa kwa urahisi, ni pamoja na nyama, samaki, na mayai, wakati vyanzo ambavyo sio nyama (kama vile maharagwe na mboga za kijani) vinaweza kuimarishwa na vyakula vyenye vitamini C ili kuongeza chuma.

Ulaji wa mboga au vyakula vya mboga

Uchunguzi kadhaa mkubwa umegundua kuwa watu wazima ambao hula matunda zaidi na mboga za majani huripoti usingizi bora, wakati wale wanaokulavyakula vya haraka zaidi (fast food) au kunywa vinywaji vya kaboni wanaripoti kupata ushingizi kwa shida zaidi.



# UTAWALA WA TRUMP,UCHUKULIWE KAMA FURSA YA KUJIKOMBOA

**UTU wetu na thamani yetu, ilishuka miaka mingi, baada ya kuukumbatia ulemavu wa kusaidiwa. Tukubaliane waafrica, kuna ujinga fulani tumeushikilia, tungekuwa watu wa kuendelea kupitia misaada, tungeshatoka hapa tulipo.**

Ukweli ni kwamba, misaada mingi ya magharibi haijawasaidia walengwa wa misaada hiyo zaidi ya kuishia mifukoni mwa watu wachache. Nitamshangaa Prof.Anna Tibaijuka, kuulizia Ukimwi ulianzia wapi?.Ukimwi ulianzia Marekani,Kama ulianzia huko, ni kwa nini Umeua na kuteketeza waafrica wengi zaidi??.

Motive ya kutengeneza,hivi virusi ilikuwa ni nini?.

Ukiisoma, na kuielewa Sayansi ya Kirusi kinavyoingia,kuathiri Chembe hai ya kinga ambayo ni ( Commander in chief), inayotoa amri, kwa chembei kinga nyingine, Lazima ukubaliane nami kuwa, maarifa ya binadamu ya " Genetic engineering yalifanya kazi.Dunia ina mengi ya kushangaza, Ngoja tujadiri tutawasaidiaje ndugu zetu wanaohitaji dawa hizi.

1) Kwa waafrica wote hii ni agenda yetu sote.a) Tu mobilise Resources,zetu tuwe na ushirika na wenye kupenda ushirika nasi, tujenge viwanda vyetu vya madawa, hata ikibidi kuwapeleka wana wa kiume na wa kike wa kitanzania, Kenya na nchi nyingine kupata maarifa ya juu zaidi ya kinga mwili( immunology).

b) Kila nchi inaweza kubeba jukumu moja moja, wakati Kenya wana tengeneza chanjo, sisi tujenge viwanda vya ARV.

2) Tuweke nguvu kwenye kukinga zaidi.a) Panaweza kuwa na vipimo vya kucheck kabla watu hawajaingiliana.b) Tutengeneze viwanda vya kuzalisha Condom nyingi.

C) Mtu anposhtuka kayatimba, basi guest zote ziwe na dawa za kuzuia kirusi hicho kusambaa( Post exposure prophylaxis).

d) Ngono duniani kote baadhi ya maeneo imekuwa ni commodity, basi kuwe na Priority kwenye nchi za kusaidia makundi yaliyoathirika kiuchumi, wapewe mikopo nafuu( serving disadvantaged societies),Ili ku shift equilibrium ya biashara ya ngono, kuja kwenye biashara nyingine.

3) 1,2, hapo juu zinaweza ku apply kama long term plan, short term plan ni kama hizi.a) Tupunguze matumizi.

Badala ya magari ya mil 600, tununue magari ya mil 60!, b) Tuwe na mfuko wa Taifa wa Ukimwi i) 10% ya mauzo ya kodi yaende kwenye mfuko huu.

ii)Tuhamasishe matumize ya Teleconference, badala ya kulazimisha watu kusafiri kwa kuchoma mafuta ya petrol kwa ma V8 ili tuwe na hela ya emergency kwa ajili ya mfuko huu, badala ya kuitumia kununulia mafuta ya magari.

iii) 7% ya mapato ya mashindano yote kwenye mpira iende kwenye mfuko wa Taifa wa Ukimwi. Ninajaribu kuonyesha tu kuwa, hili tatizo liko ndani ya uwezo wetu!, Trump kutunyima misaada, ni NIA njema, ya kutaka tushtuke, tutumie raslimali zetu kwa faida ya watu wetu na si vikundi vya watu.

TUKATAE ULEMAVU WA KUSAIDIWA.

Isaya.






# FAHAMU NAMNA WAFUNGWA WALIVYOTUMIANJIA ZA KUSHANGAZA KUTOROKA GEREZANI

**GEREZA likiwa na ulinzi mkali. Wafungwa watatu wanaohusishwa na ugaidi walitoroka gereza la kamiti nchini Kenya mwaka 2018. Watatu hao Musharaf Abdalla maarufu Alex Shikanda,Joseph Ouma na Mohammed Ali Abikar na Alhamisi walikamatwa katika eneo la Kitui.**

Walitoroka kutoka jela inayolindwa zaidi baada kutoboa ukuta wa jela hiyo.

Baadaye walitumia nguo aina ya blanketi na waya kutengeneza kamba ambazo walitumia kupanda kuta mbili ndefu za jela hiyo.

Lakini Musharaf, Joseph na Ali Abikar si watu wa kwanza kutoroka gerezani. Hapa kuna hadithi zingine za kushangaza za kutoroka gerezani ulimwenguni.

Kitendo cha kutoroka jela cha Mfaransa mmoja kwa jini la Redoine Faid mwaka 2018 ni kama hadithi . Redoine Faid - ambaye alitoroka kwa helikopta baada ya kujihami kwa silaha - aliripotiwa kuwa shabiki wa filamu za uhalifu za Hollywood.

Faid aliwahi kusema mtindo wake wa maisha umeigizwa na majambazi wanaochezwa na Robert de Niro na Al Pacino. Alikuwa akitumikia kifungo cha miaka 25 kutokana na kushiriki kwake katika wizi ambao hakufanikiwa ambapo afisa wa polisi aliuawa mwaka 2010.Alipata sifa mbaya nchini Ufaransa baada ya kutoroka jela kwa wiki sita mnamo 2013.

Polisi wenye silaha

Nchini Ugiriki mfungwa mmoja alitumia helikopta kutoroka kutoka kwa gereza lenye ulinzi mkali si mara moja, lakini mara mbili - mwaka 2006 na 2009.

Ndege zisizo na rubani pia zinakuwa hatari kwa usalama kwa magereza kote ulimwenguni - ripoti zinasema huenda zilitumika kabla ya kutoroka kwa Faid.

Mnamo mwaka wa 2017, mteka nyara aliyepatikana na hatia Jimmy Causey aliweza kutoroka kutoka kwa gereza la South Carolina kwa kutumia vikata waya na simu za mkononi.

Siagi inayonata

Wafungwa kumi na wawili walitoroka katika jela ya kaunti ya Alabama mnamo 2017 baada ya kutumia siagi ya karanga kumlaghai mlinzi ili afungue mlango unaoelekea nje.Wanaume hao walimchanganya mfanyakazi mpya kwa kupaka siagi juu ya namba kwenye mlango wa kutokea.

Joaquin 'El Chapo' Guzman

Mmoja wa watoro wa gerezani wanaojulikana sana katika historia. Ni Joaquin "El Chapo" Guzman. Mlanguzi huyu wa dawa za kulevya alizipa hekaheka jela mbili za Mexico zenye ulinzi mkali. Mnamo mwaka wa 2001 aliripotiwa kutoroshwa kutoka chini ya ulinzi ndani ya kikapu cha nguo chafu - Alikwepa kukamatwa tena kwa miaka 13 mingine.

Baada ya kurejeshwa gerezani, alitoroka tena kupitia shimo la bafuni mnamo mwaka 2015. Mfumo wa handaki wenye umbali wa maili moja ulikuwa umejengwa chini, ukiwa na taa, uingizaji hewa na reli kwa ajili ya pikipiki.

Joaquin Guzman Loera,aliyejulikana kwa jina 'El Chapo' akipelekwa gereza lenye ulinzi mkali El Altiplano, Mexico City Januari 2016.Kwa aibu zaidi ya mamlaka ya Mexico, kitendo cha El Chapo cha kutoweka kilinaswa kwenye CCTV.

Baada ya miezi kadhaa ya kukimbia - na mahojiano na mwigizaji wa Hollywood Sean Penn - Guzman hatimaye alikamatwa tena katika jimbo la Sinaloa. Kulikuwa na uvumi kwamba alitoroka tena mnamo mwaka 2016 - taarifa ambazo zilikanushwa. Alikuwa chini ya ulinzi wa Marekani akisubiri kufikishwa mahakamani wakati huo kujibu mashtaka ya dawa za kulevya baada ya kurejeshwa nchini humo.

Alivaa viatu vya visigino virefu na nguo za mkewe

Mnamo 2012, mlanguzi wa dawa za kulevya Ronaldo Silva, 39, aliripotiwa kutoroka katika gereza moja nchini Brazil kwa kubadilishana nguo na mkewe wakati alipomtembelea.Silva alivaa nguo za mkewe kabla ya kutoroka.

Baada ya kuripotiwa kunyoa na kupaka lipstick, alinaswa tena baada ya kuonekana akihangaika kutembea na viatu vya visigino virefu kwenye kituo cha basi kilicho karibu.Picha ziliibuka akiwa amevalia vazi hilo, likiwemo wigi, baada ya kurudishwa gerezani.


'Houdini raia wa Korea Kusini'

Choi Gap-bok alipata umaarufu nchini Korea Kusini baada ya kutoroka kizuizini katika mkoa wa Daegu mnamo 2012. Mtaalamu mazoezi ya yoga, alitoka akiwa amejipaka mafuta ili aweze kupita kwenye dirisha la sentimeta 15 kwa 45 lililokusudiwa linatumika kupitishia chakula.

Wachunguzi walisema mwanaume huyo mwenye uzani wa kilo 52)na futi 5 kwa inchi 1.7 alitoroka kwa chini ya dakika moja kwa "akipenya kwa urahisi mithili ya pweza".Mzee huyo mwenye umri wa miaka 50 alikamatwa tena baada ya siku sita . Kisha alifungiwa kwenye seli na sehemu ndogo ya kupitisha chakula, isiyoweza kuingilika.



# SIDHANI KAMA TUNAMTENDEA HAKI MZAMIRU YASSIN SELEMBI




HUSNA SUDI NASSORO

**NIMEWAHI kumuona Mzamiru Yassin akiwa katika jezi ya Mtibwa Sugar enzi zile. Alikuwa kiungo mahiri.Katika eneo lake Mtibwa Sugar walikuwa na utitiri wa viungo mahiri. Nyakati zile walikuwepo Mohamed Ibrahim 'MO', Mussa Nampaka, Shaban Nditti, lakini timu ilicheza kwa kumzunguka Mzamiru. Shiza Kichuya alikuwa staa, lakini hakuwahi kufanya kazi za Mzamiru wakati ule wako pamoja Mtibwa Sugar.**

Mzamiru yule wa Mtibwa Sugar ameongezeka ubora na thamani akiwa na jezi ya Simba tangu ajiunge na Wekundu wa Msimbazi. Siku zake za kwanza na Simba aliifanya kazi hii anayoifanya leo lakini katikati aliwahi kupotea kidogo akarudi tena na amebaki kwenye ubora wake mpaka sasa.

Anafanya kazi kubwa katikati mwa uwanja.Anapora mipira,anatembea sana kiwanjani. Kama tungekuwa na michoro, Mzamiru ndiyo angekuwa amechora eneo kubwa la kiungo la Simba.

Changamoto kubwa aliyonayo Mzamiru, mashabiki wa mpira nchini hawajawahi kumuelewa anachokifanya kiwanjani.Awe na jezi ya timu ya Taifa awe na jezi ya Simba hawamuelewi. Sijui kwanini.Inatokea katika maisha.

Mara nyingi wanamuona kama kiungo wa hovyo anayecheza kwa kupendelewa na makocha. Hawaoni mchango wake. Ni mara chache kukuta kundi la mashabiki limesimamia sehemu moja kumkubali Mzamiru.Ni mara chache mno kuliona hili, lakini kuona kundi hilo limegawanyika kuhusu kiwango chake ni suala la kawaida tu.

Kazi hii anayoifanya Mzamiru, ingesifiwa kama ingekuwa inafanywa na baadhi ya wachezaji wengine wa Simba au Taifa Stars.Kila siku tungesikia wakimwagiwa sifa kemkem.Lakini kwa Mzamiru ni kama hakuna anachokifanya. Nasikia mwenyewe hajali sana jinsi anavyotazamwa.

Katika timu yenye utajiri wa viungo mahiri, lakini bado nafasi yake iko kikosini. Kupata nafasi ya kucheza katika eneo la kiungo la Simba kwa miaka ya hivi karibuni si kazi ndogo. Ni kazingumu inayowashinda watu wengi.

Lakini Mzamiru amekuwa mchezaji anayecheza na kufanya kazi kubwa, lakini hatajwi sana vinywani mwa mashabiki.Kazi hii anayoifanya Mzamiru leo, haijaja katika njozi. Kuna kitu cha ziada amekifanya katika viwanja vya mazoezi. Kitu hicho marafiki zangu wengi hawana. Kibaya zaidi hawataki hata kujifunza.

Siku ambayo Mzamiru atakosekana katika kikosi cha Simba kwa michezo kadhaa, tunaweza kukaa mbele ya runinga zetu na kuziona Simba mbili tofauti. Tutaiona Simba yenye Mzamiru ndani yake na tutapuuza kama tunavyopuuza sasa, lakini tutaiona Simba iliyomkosa Mzamiru, kisha tutajua Mzamiru ni mwanaume wa kiwango gani.

kumekucha @kumekucha @kumekucha
mwanzo mpya
KUMEKUCHA



# REKODI ZA CLEMENT MZIZE ZINATISHA

NA MWANDISHI WETU

Hazungumzwi sana, lakini rekodi alizonazo ndani ya kikosi cha Yanga zinambeba, Clement Mzize aliyegeuka kuwa mshambuliaji hatari na muhimu wa kikosi hicho kilichopo chini ya kocha Sead Ramovic.

Mshambuliaji huyo mzawa licha ya kuletewa mastaa wengi wa kigeni ndani ya timu hiyo, bado ameonekana kuuwasha na kubeba rekodi nzuri kuliko mastaa hao anaocheza nao nafasi moja Jangwani.

Akiwa na msimu wa tatu tangu alipopandishwa akitokea timu ya vijana, Mzize amezidi kuwa mtamu akimfunika hadi Kennedy Musonda anayelingana muda wa kuitumikia timu hiyo, akipita mikononi mwa makocha Nasreddine Nabi na Miguel Gamondi kabla ya kuja kwa Sead Ramovic.

Katika misimu mitatu ya Ligi rekodi zinaonyesha Mzize amemkimbiza Musonda ambaye amekuwa akiimbwa kwenye kikosi hicho, kwani amehusika katika mabao 25 (kabla ya mechi dhidi ya Fountain Gate FC), akifunga mabao 16 na asisti tisa, wakati Musonda akifunga jumla ya mabao 11 na asisti mbili ndani ya misimu hiyo mitatu kwa Ligi Kuu.

Katika msimu wa Mzize wa kwanza wa 2022/23 alikuwa sehemu ya kikosi kilichoipa timu hiyo taji la Ligi Kuu akifunga mabao matano na kutoa pasi moja iliyozaa bao, hivyo alihusika kwenye mabao sita kati ya mabao 43 yaliyofungwa na timu hiyo huku Fiston Mayele (Yanga) na Saidoo Ntibanzonkiza (Simba) wakiibuka wafungaji bora baada ya kupachika mabao 17 kila mmoja.

Kwa Musonda rekodi zinaonyesha msimu huo akiingia katika dirisha dogo, alifunga mabao manne bila ya asisti, ilihali katika msimu wao wa pili, Mzize alifunga mabao sita na kuasisti saba, akimuacha mbali Mzambia huyo aliyefunga mabao matano na asisti mbili.

Kwa msimu huu wakati Musonda ndio kwanza akianza kurejea tena kutoka kwenye majeraha ana mabao mawili bila ya asisti, wakati Mzize akiwa ameshafunga mabao matano na asisti moja (kabla ya mechi ya jana), japo kwa rekodi za mechi za kimataifa kwa misimu hiyo mitatu wawili hao hawachekani, japo Mzambia ametisha zaidi.




## SIMBA WAMPA 5 FADLU

NA ELLY SARONGO

**PONGEZI KWAKE! Simba imempongeza kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids na kusema, alichofanya katika mchezo wa juzi dhidi ya Kilimanjaro Wonderers alifanya kitu kizuri zaidi kwa kuwaamini wachezaji wake.**

Juzi, Simba ilikutana na Kilimanjaro Wonderers katika mchezo wa Kombe la Shirikisho la TFF, uliopigwa katika Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salam ambapo iliondoka na ushindi wa mabao 6-0 na kufanikiwa kuingia Raundi ya 32 Bora.

Akizungumza mara baada ya mchedzo huo, Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally alisema Fadlu amefanya kitu kizuri kwa kuwaamini wachezaji wake na kuwapa nafasi ya kucheza katika mchezo huo.

"Kwanza napenda kumpongeza Fadlu kwa kuwaamini wachezaji wake wote na kuwapa nafasi katika mchezo huu, pia huu ulikuwa mchezo muhimu kwa mashabiki ambao walikuja kuwapa shukrani wachezaji wao.

="Unajua timu imecheza mechi tatu na mashabiki hawakupata fursa ya kuwaona wachezaji wao, tulicheza Tunisia, Angola tukaja mechi ya Dar es Salaam na mechi zote tatu hizi hatukuwaona wachezaji wetu.

"Tunisia hatukuwepo, Angola hatukuwepo na Dar es Salaam tulikuwa tumekula ubaya ubwela, hivyo mashabiki walikuja ili kuwapongeza wachezaji wao kwa kazi kubwa waliyofanya."